




Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa Lishe 2021/22- 2025/26



Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa Lishe 2021/22- 2025/26

1. Utangulizi

Serikali kwa kushirikiana na wadau imeandaa na kuzindua Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa masuala ya Lishe. Mpango huu umeandaliwa ili kutoa muongozo kwa wadau wote katika ngazi na nafasi mbalimbali kuhusu utekelezaji wa afua zinazolenga kutatua changamoto za lishe duni (utapiamlo) zinazoathiri watu wa rika zote katika jamii ya Watanzania. Mpango unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano yaani 2021/22 hadi 2025/26.

2. Changamoto za Utapiamlo Nchini

Mpango huu umeandaliwa kwa kuzingatia kwamba nchi yetu kwa sasa inakabiliwa na matatizo makuu ya aina tatu za utapiamlo ambayo ni

- i. Utapiamlo unaosababishwa na upungufu wa Virutubishi
 - ii. Utapiamlo unaosababishwa upungufu wa vitaminini na madini
 - iii. Utapiamlo unaosababishwa na virutubishi vinavyozidi

Matatizo haya yana athari kubwa kwa mtu mmoja-mmoja, kaya, jamii na Taifa kwa ujumla wake na hivyo kuchangia kupungua kwa kasi katika kufikia malengo yetu ya maendeleo; kiafya, kiuchumi na kijamii.



I. TATIZO LA UTAPIAMLO UNAOSABABISHWA NA UPUNGUFU WA VIRUTUBISHI

Tatizo hili linabainishwa kwa viashiria vitatu vikuu ambavyo ni udumavu, uzito pungufu na ukondefu. Mathalani, tatizo la udumavu kwa watoto wa chini ya miaka mitano bado ni kubwa sana nchini kwa mijibu wa vigezo vyta Shirika la Afya Duniani (WHO). Kipaumbibe chetu kwa mujibu wa mpango huu ni kuhakikisha tatizo hili linapungua kutoka 32% ya watoto walio na umri chini ya miaka mitano hadi 24% ifikapo mwaka 2025; na kuendelea kushuka hadi kufikia kiwango kinachokubali-ka kimataifa yaani chini ya 20%.

Kwanini Udumavyu ni tatizo?

Udumavu una athari kubwa kwenye ukuaji wa mwili na akili ya mtoto hivyo (kwa watoto) kuchangia maendeleo duni shulenii, uwezo mdogo wa kufikiri na kuelewa jambo, (kwa watu wazima) uwezo mdogo katika ubunifuna changamoto za ufanisi katika kazi (kazi za uzalishaji zisizo na tija). Vilevile, idadi ya watoto waliodumaa ni zaidi ya milioni 3,000,000 na idadi hii inazidi kuongeze-ka mwaka hadi mwaka.

“Kwa wastani hivi sasa nchini Tanzania katika kila watoto 10 wenye umri chini ya miaka mitano watoto 3 wamedumaa”.



II. TATIZO LA UPUNGUFU WA VITAMINI NA MADINI

Tatizo hili linabainishwa na hali ya upungufu wa madini chuma na foliki, madini joto na vitaminini A. Upungufu wa madini chuma na foliki unapelekea watoto kuzaliwa na tatizo la mgongo wazi na wengine vichwa vikubwa, upungufu wa damu kwa watoto wa chini ya miaka mitano, vijana balehe hasa wasichana na wanawake walio katika umri wa kuzaa.

Kwa nini upungufu wa damu ni tatizo?

Tatizo la upungufu wa damu lina madhara makubwa hasa kwa kinamama wajawazito kwani huchangia uwezekano wa kujifungua watoto njiti na hata vifo kwa mama na mtoto wakati wa kujifungua. Kwa vijana na watoto changamoto hii inasabisha udhaifu wa mwili, hali ya mwili kuchoka, kutokamilisha majukumu kwa wakati na kuongeza uwezekano wa kupata magonjwa. Kipaumbele chetu ifikapo mwaka 2025 ni kuhakikisha tatizo hili linapungua mionganoni mwa kina mama kutoka 29% hivi sasa hadi 23% na kuendelea kupunguza tatizo la upungufu wa vitamini A kwa watoto kutoka 33% hadi kufikia 20%.

“Nchini Tanzania katika kila wanawake 10 wanawake 3 wana tatizo la upungufu wa damu. Pia, katika kila watoto 10 watoto 6 wana tatizo la upungufu wa damu”



III. TATIZO LA UZITO ULIOZIDI NA KIRIBATUMBO


Serikali kwa kushirikiana na wadau imeandaa na kuzindua Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa masuala ya Lishe. Mpango huu umeandaliwa ili kutoa muongozo kwa wadau wote katika ngazi na nafasi mbalimbali kuhusu utekelezaji wa afua zinazolenga kutatta changamoto za lishe duni (utapiamlo) zinazoathiri watu wa rika zote katika jamii ya Watanzania. Mpango unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano yaani 2021/22 hadi 2025/26.

Kwa nini uliozidi na kiribatumbo ni tatizo?

Kwa kiasi kikubwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza (kisukari, figo, shinikizo la juu la damu, magonjwa ya moyo na baadhi ya saratani) yanahusishwa zaidi na mitindo ya maisha hususan ulaji usiofaa. Aidha, gharama za matibabu kwa magonjwa haya huwa ni mzigo mkubwa sana kwa mtu binasfi, kaya na Taifa kwa ujumla. Vilevile, waathirika wa magonjwa haya

wanalazimika kuendelea na matibabu katika kipindi chote cha uhai wao. Idadi ya waathirika ni kubwa (zaidi ya wanawake 3.3 milioni) na inaendelea kuongezeka kila mwaka. Kwa wajawazito walio katika kundi hili athari kubwa ni kupata kifafa cha mimba wakati wa kujifungua na hivyo kuhatarisha maisha yao na mtoto.

“Hivi sasa, kati ya watu 10, watatu (3) wana uzito uliozidi au kiribatumbo na mtu 1 kati ya watu 10 ana tatizo la kisukari.”



3. MBINU ZITAKAZOTUMIKA KATIKA KUKABILIANA NA MATATIZO YA LISHE

3.1 Utekelezaji wa afua zinazolenga watu wa rika zote

Ili kuhakikisha kuwa hakuna anayeachwa nyuma, Mpango huu unalenga kutatta matatizo ya lishe yanayokabili watu wa rika zote yaani kuanzia kipindi cha ujauzito, watoto, vijana, watu wazima na wazee. Aidha, watu wenye mahitaji maalum ya lishe nao wamezingatiwa mfano wenye magonjwa yasiyo yakuambukiza, waishio na Virusi vya UKIMWI, wale mavu, n.k. Hivyo, afua muhimu za kukabiliana na utapiamlo kwa rika zote zimeainishwa kwenye Mpango huu.

AFUA ZINAZOLENGA WATU WA RIKA ZOTE



Wajawazito na Wanaonyonesha

- . Kuhamasisha Matumizi ya Madini Chuma na Vitamini vya Foliki
- . Kuhamasisha ulaji wa vyakula mchanganyiko
- . Kufanya tathmini ya hali ya lishe
- . Kuhamasisha kupata huduma sahihi za afya

- . Kuhamasisha Ulaji wa Vyakula Mchanganyiko
- . Kufanya tathmini ya hali ya lishe
- . kutoa elimu na unasihi wa lishe
- . Kuhamasisha mtindo bora wa maisha

**Watu Wazima umri
miaka 60 na zaidi**

- . Kuhamasisha ulishaji sahihi
- . kutoa matibabu ya Utapiamlo
- . Kufanya ufuutiliaji wa ukuaji na maendeleo
- . Utoaji wa virutubishi kwa watoto.

**Watoto umri miezi
0 hadi 59**

**Wanawake na
Wanaume
umri miaka 20-59**

- . Kuhamasisha Ulaji wa Vyakula Mchanganyiko
- . Kufanya tathmini ya hali ya lishe
- . kutoa elimu na unasihi wa lishe
- . Kuhamasisha mtindo bora wa maisha

**Watoto umri
miaka 5-9
vijana 10-19**

- . Kuhamasisha Ulaji wa Vyakula Mchanganyiko
- . Kufanya tathmini ya hali ya lishe
- . Kutoa elimu na unasihi wa lishe
- . Kutoa matibabu ya Utapiamlo

3.2 Utekelezaji wa afua kupitia Mifumo ya kisekta

Kwa kutambua kuwa mifumo mbalimbali inachangia kwa kiasi kikubwa kwenye matokeao ya lishe, Mpango huu umeainisha mifumo mitano (5);

- 1. Mfumo wa Upatikanaji wa Chakula,*
- 2. Afya,*
- 3. Maji na Usafi wa Mazingira,*
- 4. Kinga ya Jamii na*
- 5. Maji.*

Mifumo hii inachangia kuimarisha hali ya lishe kwa mtu mmoja-mmoja na jamii kwa ujumla. Matumizi ya mifumo hii yanaendelea kudhihirisha azma ya Serikali kuhakikisha kuwa wadau wa sekta mbalimbali wanashiriki kikamilifu katika harakati za kitaifa za kukabiliana na chanagamoto za utapiamlo.

3.3 Mfumo wa Upatikanaji Wa Chakula

Mpango huu unalenga kuboresha utekelezaji wa afua za lishe kupitia sera, miongozo, programu, na upatikanaji wa huduma bora ili kuhakikisha mfumo mzima wa chakula unakuwa endelevu na wenye manufaa zaidi katika kufikiwa kwa malengo ya mpango.



Vilevile, mpango huu unakusudia kuimarisha mnyororo mzima wa chakula utakaowezesha upatikanaji rahisi wa vyakula mchanganyiko, salama, vya kutosha, na kwa gharama nafuu.




Kupitia mpango huu, wadau wote katika mfumo wa chakula ikiwemo wazalishaji, wasindikaji, wasambazaji na wauzaji wanaelekezwa kuzingatia upatikanaji wa chakula kilicho salama kwa watu wote ikiwa ni pamoja na makundi maalum kama vile watoto, vijana balehe, wajawazito na wazee, ili kulinda afya zao.

Aidha, mpango unahimiza kuzingatiwa kwa mazingira salama ya chakula yanayohamasisha ulaji unaofaa, kwa mfano, kudhibiti matangazo yanayohamasisha ulaji wa vyakula vyenye wingi wa sukari, chumvi na mafuta.

3.4 Mfumo wa Afya

Mfumo wa afya unahusisha utoaji wa huduma, uwepo wa rasilimali watu, fedha, upatikanaji wa vifaa tiba na uratibu, ili kuhakikisha watu wote wanakuwa na afya bora.

Mpango huu unalenga kuboresha utekelezaji wa afua za lishe kupitia sera, mipango, usimamizi, upatikanaji wa huduma bora na mazingira wezeshi katika mfumo mzima wa afya. Mfumo madhubuti wa afya utachangia kuimarisha upatikanaji wa huduma kama vile unasihi wa lishe, kutoa matibabu kwa watu wenye utapiamlo, na kuhamasisha tabia chanya zinazoboresha lishe



Aidha, mpango unakusudia kuendelea kuhamasisha matumizi ya huduma za chanjo, huduma bora za afya na lishe kwa watoto, wajawazito na wanawake waliojifungua na makundi mengine, kupitia vituo vya kutolea huduma na katika jamii.

3.5 Mfumo wa Maji na Usafi wa Mazingira

Mpango huu unalenga kuboresha utekelezaji wa afua za lishe kupitia sera, mipango, usimamizi, upatikanaji wa huduma bora na mazingira wezeshi katika mfumo wa maji na usafi wa mazingira unahusisha sera, mipango na programu zinazohusu upatikanaji na matumizi ya maji safi na salama, usafi wa mazingira na usafi binafsi kwa jamii nzima.

Ili kuondoa utapiamlo wa aina zote, mfumo wa maji na usafi wa mazingira ni muhimu kwa upatikanaji wa chakula salama na kuwezesha mwili kufyonza ipasavyo virutubishi vilivyomo kwenye chakula. ka mfumo mzima wa afya. Mfumo madhubuti wa afya utachangia kuimarisha upatikanaji wa huduma kama vile unasihi wa lishe, kutoa matibabu kwa watu wenye utapiamlo, na kuhamasisha tabia chanya zinazoboresha lishe katika kaya na jamii kwa ujumla.



Usafi binafsi na mazingira safi na salama humlinda mtu kutohakikisha na magonjwa kama vile kuhanisha na minyoo; magonjwa ambayo yanaweza kusababisha utapiamlo

Mpango huu unalenga kuhimiza uwepo na matumizi ya mazingira wezeshi ya upatikanaji wa uhakika wa maji safi na salama, uwepo na matumizi sahihi ya vyoo bora na kuhamasisha usafi wa mazingira.

3.6 Mfumo wa Kinga ya Jamii

Mfumo wa kinga ya jamii unajumuisha sera na mipango yenye lengo la kuhakikisha kuwa jamii hususanii makundi maalum inalindwa kutoka kwenye umaskini uliokithiri.

Mfumo madhubuti wa kinga ya jamii unawezesha makundi yenye uhitaji maalum kupata huduma na mahitaji ya msingi.



Mpango huu unalenga kuimarisha matumizi thabiti ya mfumo wa kinga ya jamii kuwezesha kaya na watu wenye mahitaji maalum kwa mfano wazee, wajawazito, watoto chini ya miaka mitano, na watu wenye ulemau kupata huduma muhimu za lishe ili kuondokana changamoto za tatizo la utapiamlo.

3.7 Mfumo wa Elimu

Mfumo huu unajumuisha sera, mipango, programu, wadau wanaohusika na utoaji huduma ya elimu ili kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora kwa jamii.

Mfumo madhubuti wa elimu utasaidia upatikanaji wa elimu katika ngazi zote kuanzia elimu ya awali hadi vyuo vikuu, ili kuwezesha watoto na vijana kupata elimu na ujuzi sahihi.

Mpango huu unalenga kutumia mfumo wa elimu kuhamasisha masuala ya lishe, ambapo mfumo huu utatumika kama jukwaa la kuchochea mabadiliko ya tabia ili kuwezesha kupata matokeo bora ya lishe hususan kwa vijana.



Mfumo madhubuti wa elimu utawezesha wahusika wa kundi hili kutambua umuhimu wa lishe bora na mtindo bora wa maisha katika mazingira yao.

4. Maeneo ya Matokeo katika utekelezaji wa Mpango

Mpango huu umelenga kuona matokeo katika maeneo makubwa manne (4) kama ifuatavyo: -

- i. *Kupunguza utapiamlo unaotokana na upungufu wa virutubishi (udumavu, uzitopungufu, ukondedefu)*
- ii. *Kupunguza tatizo la upungufu wa vitaminini na madini*
- iii. *Kupunguza na kudhibiti tatizo la uzito uliozidi na kiribatumbo*
- iv. *Kupunguza na kudhibiti tatizo la uzito uliozidi na kiribatumbo*

5. Matokeo ya kimkakati

Ili kufikia matokeo tarajiwa, mpango huu umeainisha matokeo matano (5) ya kimkakati ambayo ni: -

5.1 Ongezeko la Upatikanaji wa Huduma za kutosha za Lishe zenye Ubora na kwa Usawa

Mpango huu unalenga kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za lishe ikiwemo upatikanaji wa vyakula dawa, virutubishi vyta nyongeza na vitendea kazi vyta lishe kwa mfano vifaa vyta kutathmini hali ya lishe. Aidha, mpango huu utaimarisha upatikanaji wa huduma kwa jamii kwa kuzijengea uwezo taasisi mbalimbali ambapo utekelezaji wa afua za lishe unafanyika. Vituo na taasisi hizi zinajumuisha vituo vyta kutolea huduma za afya, shule, magereza, maeneo ya kazi na vituo vyta malezi na makuzi.

5.2 Ongezeko la Wanawake, Wanaume, Watoto na Vijana Wanaotekeleza Tabia Chanya za Lishe

Ili kuweza kufanikisha hili, mpango huu utahakikisha kuwa watu wa rika zote wana uelewa, ujuzi na rasilimali stahiki za kuwawezesha kutekeleza tabia chanya za lishe. Baadhi ya tabia zinazohamasishwa ni zile zinahusiana na ulishaji sahihi wa watoto, ulaji unaofaa, matumizi sahihi ya virutubishi pamoja na utumiaji wa huduma za afya na usafi wa mazingira.

5.3 Uwepo wa Mifumo Endelevu Na Himilivu ya Upatikanaji wa Chakula inayokidhi Mahitaji ya Lishe

Mpango huu unalenga kuimariswa kwa utekelezaji wa afua za lishe katika mnyororo wa thamani wa chakula kwa kuhamasisha na kujenga uwezo wa wadau, na kuhamasisha uimariswaji wa miundo mbinu ya upatikanaji wa chakula. Mpango huu unalenga pia kuchochaea na kuhamasisha matumizi ya teknolojia ili kuhakikisha upatikanaji wa vyakula mchanganyiko, salama na vyenye virutubishi vya kutosha. Aidha, mpango huu unalenga kuimariswa mazingira yanayohakikisha na kuchochaea ulaji unaofaa.

5.4 Kuimariika kwa Ushiriki wa Kisekta pamoja na Sekta Binafsi kwenye Masuala ya Lishe

Mpango huu unakusudia kuongeza ushiriki wa wadau wa kisekta hususani sekta binafsi katika kusaidia na kuchangia utoaji wa huduma za lishe kwa kuainisha wajibu na majukumu na kuwajengea uwezo wahusika katika kutekeleza afua za lishe. Aidha, mpango unalenga kuongeza wigo wa wadau wa sekta binafsi wanaoweza kuchangia utoaji wa huduma za lishe katika maeneneo mbalimbali nchini.

5.5 Kuimariika kwa Mazingira Wezeshi ya Lishe

Mpango huu unakusudia kuendelea kuimariswa kwa mazingira wezeshi kupitia uratibu madhubuti wa kisekta katika ngazi zote, kuhamasisha uongozi na mwitikio wa kisiasa kwa masuala ya lishe, kuweshera upatikanaji wa rasilimali watu na fedha, kuboresha upatikanaji na utumiaji wa taarifa na takwimu za lishe na kusimamia utekelezaji wa sera, mikakati, programu na miongozo ya lishe.

6. Shabaha za Mpango kwa kipindi cha miaka mitano (5)

	Kiashiria cha Matokeo	Kiwango cha Sasa	Shabaha (2025/26)
1.	Kupunguza kiwango cha udumavu kwa watoto wenye umri kati ya miezi 0-59.	31.8% (2018)	24%
2.	Kudhibiti kiwango cha ukondefu kwa watoto kati ya miezi 0 -59.	3.5% (2018)	<5%
3.	Kupunguza kiwango cha watoto wanaozaliwa na uzito pungufu.	6.3% (2018)	<5%
4.	Kupunguza kiwango cha upungufu wa damu kwa wanawake walio na umri wa kuzaa kati ya miaka 15 – 49.	28.8% (2018)	23%
5.	Kupunguza kiwango cha upungufu wa vitaminini A kwa watoto wa umri kati ya miezi 6 hadi 59.	33% (2010)	20%
6.	Kudhibiti kiwango cha madini joto kwenye mkojo kwa wanawake walio na umri wa kuzaa kati ya 100 – 299 $\mu\text{g}/\text{L}$	100-299 $\mu\text{g}/\text{L}$ (2010)	100-299 $\mu\text{g}/\text{L}$
7.	Kudhibiti kiwango cha uzito uliozidi kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.	2.8 (2018)	<5%
8.	Kudhibiti kiwango cha uzito uliozidi au kiribatumbo kwa wanawake wenye umri wa miaka 15 -49.	31.7% (2018)	<32%
9.	Kudhibiti kiwango cha uzito uliozidi kwa watu wazima.	26% (2012)	<30%

7. Ufutiliaji na Tathmini

Ili kuhakikisha kuwa matokeo tarajiwa yanafikiwa, Mpango umejiwekea utaratibu wa kufanya ufutiliaji na tathmini kila baada ya robo mwaka, mwaka, katikati na mwishoni mwa utekelezaji ili kupima maendeleo ya

Hii itawezesha kupata taarifa za utekelezaji, kuainisha mafanikio na changamoto ili kujifunza na kufanya maboresho maeneo yanayohitajika. Jukwaa la pamoja la Taarifa na Takwimu za lishe (Multisectoral Nutrition Information System – MNIS) pamoja na Mfumo wa Ufutiliaji na Tathmini (Integrated Monitoring and Evaluation System - iMES) vitatumika kukusanya na kutoa taarifa za utekelezaji za mara kwa mara kuititia viashiria mahususi kila mwaka. Kadi alama za lishe kwa kila robo mwaka itatumika kubaisha hali halisi katika maendeleo ya utekelezaji.

Tafiti za kitaifa kama vile Utafiti wa Taifa wa hali ya Lishe (Tanzania National Nutrition Survey - TNNS) na Utafiti wa Taifa wa Demografia na Viashiria vya Malaria Tanzania (TDHS) zitatumika kutoa matokeo ya mafanikio baada ya mwisho wa utekelezaji, kwa mujibu wa malengo na shabaha za mpango huu.

8. Uratibu katika utekelezaji

Ofisi ya Waziri Mkuu imepewa jukumu la jumla kitaifa la kuratibu utekelezaji wa afua zote za lishe ambazo zinatekelezwa kutoka Sekta mbalimbali (ndani na nje ya Serikali) ili kuhakikisha kuwa malengo na shabaha yanafikiwa ipasavyo. Katika utekelezaji wa majukumu yake ya uratibu, OWM itasaidiwa na Taasisi ya Chakula na Lishe ambayo ina jukuma la kitaalam kama chombo cha taifa cha kutoa uongozi wa kimkakati katika utekelezaji wa afua za lishe nchini. Majukumu ya Wizara, Taasisi na Mashirika ya umma nayo yamebainishwa kwa kuzingatia majukumu yao ya kimamlaka katika muundo wa Serikali. Aidha, wadau wengine ambao wanajumuisha mashirika ya kimataifa na yale ya Umoja wa Mataifa, taasisi za elimu ya juu na utafiti, asasi za kiraia na sekta binafsi wametambuliwa na utekelezaji wa kila mwaka kwa mujibu wa eneo la matokeo ni kama inavyoonekana kwenye jedwali.

9. Gharama za kutekeleza Mpango (Bajeti kwa kila eneo la matokeo)

Mpango huu wa miaka mitano (5) utatakelezwa kuititia afua za lishe za kisekta katika mifumo ya chakula, afya, elimu, maji na usafi wa mazingira na mfumo wa kinga ya jamii. Gharama za jumla katika kipindi chote cha utekelezaji ni takriban Shilingi 642,349,052,101.30 ambapo asilimia 79.9 ya fedha hizi inategemewa kupatikana kuititia vyanzo vya ndani ya nchi.

Kiasi kilichosalia kinategemewa kupatikana kuititia maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na michango ya wadau wa maendeleo na sekta binafsi, utekelezaji wa mipango na programu za kisekta za kitaifa, tozo kwenye bidhaa ambazo ni hatarishi kwa afya za walaji na mikopo nafuu kutoka mashirika ya kimataifa. Mchanganuo wa gharama za utekelezaji wa kila mwaka kwa mujibu wa eneo la matokeo ni kama inavyoonekana kwenye jedwali.

Gharama za Kutekeleza Mpango kwa Bilioni za Shilingi ya Tanzania.

Maeneo ya Matokeo	Mwaka1 2021/22	Mwaka2 2022/23	Mwaka3 2023/24	Mwaka4 2024/25	Mwaka4 2025/26
1. Kupungua Utapiamlo wa Upungufu wa Virutubishi	57.94	60.46	31.46	7.64	7.8
2. Kupungua Tatizo la Upungufuwa Vitamini na Madini	81.73	80.23	76.13	78.78	85.22
3. Kupunguza Tatizo la Uzito na Kiribatumbo	1.35	2.86	2.87	3.02	2.68
4. Kuimarisha mazingira Wezeshi	14.02	11.01	12.64	10.98	13.52
JUMLA	155.03	154.56	123.1	100.42	109.23

10. Shukrani

Kazi hii imeandaliwa na Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania kuititia Idara ya Sera na Mipango. Tunatambua mchango wa Bwana Geoffrey Chiduo (Kaimu Mkuu wa Idara), Bi. Julieth Itatiro (Mkuu wa Sehemu ya Uchambuzi wa Sera), Bi. Deborah Charwe na Bibi Neema Joshua wote kutoka katika Taasisi ambao ndio hasa walifanya kazi ya uandishi wa muhtasari huu.

Aidha , shukurani za dhati zinatolewa kwa Shirika la USAID mradi wa “Advancing Nutrition” kwa mchango mkubwa wa kitaalam uliotolewa na Bibi Deborah Niyeja na Dkt. Theresia Jumbe katika maandalizi. Tunapenda pia kutoa shukrani za kipekee kwa Shirika la USAID mradi wa “Advancing Nutrition” kwa mchango wa fedha uliowezesha kukamillisha kazi hii kwa ufanisi.



MAWASILIANO

Kwa Taarifa zaidi kuhusu Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe wa mwaka 2021/22- 2025/26 wasiliana na;

Mkurugenzi Mtendaji

**Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania,
22 Barabara ya Barack Obama.**

S.L.P 977

**11101 Dar Es Salaam, Tanzania,
Simu: +255 734275369, +255 22 2118137**